



# CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI

## MAFUNZO YA KUFUNDISHA KISWAHILI KAMA LUGHA YA KIGENI

### Malengo ya Mafunzo

Kutoa mafunzo kwa walimu watakaofundisha Kiswahili kama lugha ya Kigeni/Pili kwa kuwapatia maarifa, mbinu na ujuzi wa kuwafundisha wageni na/au kuimarisha maarifa yao.

### Maudhui ya Mafunzo

- Dhana muhimu katika ufundishaji wa lugha ya kigeni/pili
- Mikabala ya ufundishaji wa lugha ya kigeni/pili, zana na mbinu zake
- Masuala ya msingi wakati wa ufundishaji
- Ufundishaji kwa kuzingatia makundi maalumu
- Utendaji darasani na mahitaji yake
- Ufundishaji wa lugha ya kigeni/pili kwa njia ya mtandao
- Utamaduni na masuala mtambuka.

### Matokeo ya Mafunzo

Mwisho wa mafunzo haya, washiriki wanatarajiwa kuwa na uwezo wa kufundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni/pili kwa makundi na hatua mbalimbali na kwa kutumia mikabala, zana, mbinu na njia mbalimbali.

### Walengwa wa Mafunzo

Wadau wote wenye raghba ya kufundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni/pili au wanaofanya kazi hiyo na ambao wangependa kuimarisha stadi zao za ufundishaji.

### Namna ya Kujiandikisha

Bofya hapa

<https://dps.udsm.ac.tz/view?course=141>  
au tembelea [www.udsm.ac.tz](http://www.udsm.ac.tz)

### Gharama kwa Kila Mshiriki

Gharama kwa kila mshiriki ni shilingi 500,000/=.

### Muda na Njia za Ufundishaji

Mafunzo yatatolewa ana kwa ana na kwa njia ya mtandao kwa muda wa siku 10 kuanzia tarehe 13 Hadi 24 January, 2025.

### Mawasiliano

- Dkt. Salome J. Kotira – 0747 841 509. Barua pepe: [salomejerome91@gmail.com](mailto:salomejerome91@gmail.com)
- Bi. Levina Kisaka: 0736 264 282, [levina.kisaka@udsm.ac.tz](mailto:levina.kisaka@udsm.ac.tz)

### Mafunzo Yanatolewa na:

Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.